# MAONI YA WADAU KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA

# ULINZI WA TAARIFA BINAFSI, 2022

**Oktoba 19, 2022**

**Wadau husika:**

**JamiiForums | LHRC | TLS | TAMNOA | Twaweza | TBA | MultiChoice Tanzania**

Maoni haya yanawasilishwa kwa pamoja na taasisi zifuatazo;

1. Jamii Forums (JF)
2. Tanganyika Law Society (TLS)
3. Legal and Human Rights Centre (LHRC)
4. Tanzania Mobile Network Operators Association (TAMNOA)
5. Tanzania Bankers Association (TBA)
6. Twaweza
7. Tanzania Human Rights Defenders (THRDC)
8. Multichoice Tanzania

Wadau tunapongeza jitihada za kuwasilishwa kwa Mswada wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi, 2022 kwa kuwa ni sheria tuliyokuwa tukiiisubiri kwa muda mrefu n ani sheria muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Maoni ya Jumla**

- **Bodi iondolewe**. Tunapendekeza bodi iondolewe ili kupunguza Gharama za uendeshaji wa Tume inayoundwa chini ya Sheria hii. Badala yake tunapendekeza kwamba Tume isimamie shughuli zote za ulinzi wa taarifa binafsi na faragha bila kuingiliwa na mamlaka yoyote. Tunapendekeza pia kwamba Mkurugenzi akishateuliwa na kuidhinishwa na Bunge basi awajibike kwa Bunge. Hii itasaidia Tume kuwa huru na kupimwa uwajibikaji wake na Bunge.
- **Mpangilio wa sura**. Tunapendekeza kwamba Sura ya 8 iwe Sura ya 3 ili kuweka mtiririko mzuri na wenye kuleta maana.
- Tunapendekeza iwepo sehemu inayoweka utaratibu wa kufanya tathmini ya athari za kutoa taarifa (Data Protection Impact Assessment) na isomeke kama mfano uliombatanishwa hapo chini (mwishoni)
- Tunapendekeza kwamba ridhaa ya Maandishi isiishie kwenye taarifa nyeti tu; badala yake itumike kwa taarifa zote binafsi.
- Haki ya Mhusika wa Taarifa binafsi kupata nakala ya taarifa zinazokusanywa au zilizochakatwa haijaainishwa katika Muswada
- Muswada haujaweka haki ya kuomba idhini ya haki ya taarifa binafsi kuhamishwa kwenda kwa msimamizi wa mirathi au mwakilishi wa kisheria (Right of Transmission)
- Tunapendekeza kuwepo katika Sheria hii kifungu kinachosema wazi kwamba kama kuna mgongano wowote kati ya sheria nyingine na sheria hii, basi sheria hii itatamalaki kwa masuala yote ya taarifa binafsi na faragha.
- Tunapendekeza kuwepo na Masharti ya Mpito ili kuwapa wadau muda wa kujipanga kutekeleza matakwa ya sheria hii.
- Tunapendekeza maneno ‘Maslahi ya Umma’ yapewe tafsiri maalum kwa sababu yametumika mara tatu ndani ya muswada
- Tunapendekeza maneno ‘Usalama wa Taifa’ yapewe tafsiri maalum kwa sababu yametumika mara mbili ndani ya muswada
- ‘Ridhaa ya mhusika wa taarifa’ (consent) ipewe tafsiri kuepusha mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa sheria
- Uficho/faragha/kutokujulikana kwa mhusika wa taarifa (anonymization) wakati wa matumizi ya taarifa binafsi kibiashara haujapewa kipaumbele katika Muswada. Tumeambatanisha mfano wa kifungu pendekezwa hapo chini.
- Mdhibiti wa taarifa binafsi hajatajwa kokote kwenye muswada (Data Controller). Tunapendekeza aongezwe kwenye vifungu husika kama tulivyopendekeza kwenye bango-kitita. Aidha, tafsiri iwekwe kwenye kifungu cha tafsiri ya maneno.
- Kifungu cha 5 kinachozungumzia Misingi ya Ulinzi wa Taarifa hakijajumuisha Msingi wa Uwajibikaji. Tunapendekeza msingi huu uongezwe na isomeke “Mdhibiti wa Taarifa Binafsi atawajibika moja kwa moja kwa uchakataji wa taarifa binafsi ikijumuisha wachakati na wawakilishi wake wakati wa uchakataji wa taarifa binafsi chini ya maelekezo yake”
- Tunapendekeza kiongezwe kifungu kipya baada ya kifungu cha 39 kitakachotoa nafasi ya wahusika katika malalamiko kumaliza mgogoro wao nje ya utaratibu wa Tume na Mahakama ili kupunguza mrundikano wa mashauri kwa Tume. Tunependekeza kifungu hicho kisomeke kama mfano ulioambatanishwa hapo chini.
- Tunapendekeza kifungu cha 65 kibadilishwe badala ya kuweka ulazima kwa kila mkusanyaji, mchakataji na mdhibiti wa taarifa binafsi kuwa na sera ya kukusanya, kuchakata, kudhibiti na kulinda taarifa binafsi; kazi hiyo ifanywe na Tume kwa kuweka sera ya mfano (standard) ambayo itafuatwa na watajwa wote hapo juu.

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Jina la mswada**<br>Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa lengo la kuweka kiwango cha chini cha matakwa ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi zinazochakatwa na vyombo vya Serikali na vyombo binafsi, na masuala mengine yanayohusiana na hayo | Kuongeza neno Faragha ili iendane na masharti ya Katiba Ibara ya 16 na 18 ya JMT | Neno Faragha inakosekana | Sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi na faragha kwa lengo la kuweka kiwango cha chini cha matakwa ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi, kuanzisha Tume ya Ulinzi wa taarifa Binafsi, kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi zinazochakatwa na vyombo vya Serikali na vyombo binafsi, na masuala mengine yanayohusiana na hayo |
| | **Kifungu namba 1 Jina na kuanza kutumika**<br>Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya Mwaka 2022 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri atateua kwa notisi katika Gazeti la Serikali. | Muda wa kuanza kwa utekelezaji inatakiwa kuainishwa<br><br>Au sheria iamuru Waziri kutoa notice isiyopungua siku 90 | Kutoa muda kwa wadau kujiandaa ili kuepuka kuwa na sheria isiyotekelezwa | Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Faragha ya Mwaka 2022 na itaanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri atateua kwa notisi katika Gazeti la Serikali ambayo itakuwa ndani ya mwaka mmoja tangu kupitishwa kwa sheria hii. |
| | **Kifungu 3 – tafsiri**<br>“Afisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi” maana yake ni mtu aliyeteuliwa na mkusanyaji na kupewa jukumu la kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa katika Sheria hii; | Liongezwe neno ‘Mchakataji’ | Neno ‘mchakataji’ limekosekana | “Afisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi” maana yake ni mtu aliyeteuliwa na mkusanyaji au mchakataji na kupewa jukumu la kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yaliyoainishwa katika Sheria hii |
| | **Kifungu 3 – tafsiri**<br>“Kanuni za maadili” maana yake ni kanuni zinazobainisha maadili na miiko ya wachakataji na wakusanyaji wa taarifa binafsi zinazoandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 65 | Neno “wadhibiti” limekosekana | Tunaamini wadhibiti pia wanatakiwa kuzingatia maadili husika. | “Kanuni za Maadili” maana yake ni kanuni zinazobainisha maadili na miiko ya wachakataji, wakusanyaji na wadhibiti wa taarifa binafsi kama ilivyoainishwa katika nyongeza ya jedwali |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | **Kifungu 3 – tafsiri**<br>"Mchakataji" maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma ambayo inachakata taarifa binafsi kwa ajili na kwa niaba ya mkusanyaji chini ya maelekezo ya mkusanyaji, isipokuwa kwa watu ambao, chini ya mamlaka ya moja kwa moja ya mkusanyaji, wanaruhusiwa kuchakata taarifa binafsi, na itajumuisha mwakilishi wake; | Maboresho ya mpangilio wa Maneno | | "Mchakataji" maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma ambayo inachakata taarifa binafsi kwa ajili na kwa niaba ya mkusanyaji chini ya maelekezo ya mkusanyaji na itajumuisha mwakilishi wake; |
| | **Kifungu 3 – tafsiri**<br>"mahakama" maana yake ni mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza suala husika; | | Mahakama zenye mamlaka zitajwe, kwasababu zipo taasisi ambazo sio mahakama lakini zenye usuli wa kimahakama zinazoshughulika na masuala ya taarifa binafsi. | "Mahakama" maana yake ni mahakama ya mwanzo, wilaya, hakimu mkazi, mahakama kuu au Mahakama ya rufani |
| | **Kifungu 3 – tafsiri**<br>"Mhusika wa taarifa" maana yake ni mhusika wa taarifa binafsi zinazochakatwa kwa mujibu wa Sheria hii; | Upanuzi wa tafsiri | Tafsiri imepanuliwa kuipa sheria mawanda mapana na kumlinda mhusika wa taarifa kwa namna bora zaidi | "Mhusika wa Taarifa" maana yake ni mtu anayetambulika au anayeweza kutambulika moja kwa moja au vinginevyo ikiwa pamoja na anayetambulika kimtandao ambaye taarifa zake zinakusanywa, zinachakatwa au zinatarajiwa kuchakatwa. |
| | **Kifungu 3 tafsiri**<br>Mkurugenzi Mkuu | Kutolowea kwa tafsiri hii | Haileti mantiki kwa kuwa Mkurugenzi aliyetajwa kwenye sheria ni mmoja tu na ameshatajwa kwenye kifungu husika | Tafsiri hii iondolewe |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | **Kifungu 3 tafsiri**<br><br>"Mkusanyaji" maana yake ni mtu, taasisi binafsi au taasisi ya umma ambayo peke yake au kwa pamoja na taasisi nyingine huamua madhumuni na njia za uchakataji wa taarifa binafsi; na pale ambapo madhumuni na njia za uchakataji zimebainishwa katika sheria, "mkusanyaji" ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma iliyoteuliwa kwa mujibu wa sheria na itajumuisha mwakilishi wake; | | Kulikuwa na mkanganyiko wa tafsiri pendekezwa na Serikali katika Muswada wake kwa kutumia neno 'uchakataji' badala ya 'ukusanyaji' | "Mkusanyaji" maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma ambayo peke yake au kwa pamoja na taasisi nyingine huamua madhumuni na njia za ukusanyaji wa taarifa binafsi; na itajumuisha mwakilishi wake; |
| | **Kifungu 3 tafsiri**<br>"Mpokeaji" maana yake ni mtu, taasisi nafsi, taasisi ya umma au mtu mwingine yeyote ambaye anapokea taarifa binafsi kutoka kwa mkusanyaji | Kuongeza maneno 'mchakataji na mdhibiti' yanakosekana | Tunaamini maneno haya ni muhimu kwa kuwa watajwa wote wanahusika. | "Mpokeaji" maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma au mtu mwingine ambayo inapokea taarifa binafsi kutoka kwa mkusanyaji, mchakataji au mdhibiti. |
| | **Kifungu 3 tafsiri**<br>"Mtaalamu wa Afya" maana yake ni mtu anayetoa huduma za afya na kutambuliwa hivyo kwa mujibu wa sheria | Nyongeza ya neon | Neno 'Mtaalamu wa Afya' limeshatafsiriwa na sheria ya Afya, ni vyema kuirejea ili kuepuka kuwa na tafsiri isiyo rasmi. | "Mtaalamu wa Afya" maana yake ni mtu anayetoa huduma za afya na kutambuliwa hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Afya Namba 12, 2009. |
| | **Kifungu 3 Tafsiri**<br>"Mtu mwingine" maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma tofauti na- (a) mhusika wa taarifa; (b) mkusanyaji au mchakataji; na (c) mtu yeyote aliyepewa mamlaka ya kuchakata taarifa binafsi; | Nyongeza ya neon | Kuongeza 'mdhibiti' | "Mtu mwingine" maana yake ni mtu, taasisi nafsi au taasisi ya umma tofauti na- (a) mhusika wa taarifa; (b) mkusanyaji au mchakataji; (c) mdhibiti na (d) mtu yeyote aliyepewa mamlaka ya kuchakata taarifa binafsi; |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | **Kifungu 3 Tafsiri**<br>"Nyaraka" maana yake ni njia yoyote ambayo taarifa imerekodiwa, iwe imechapishwa au ipo kwenye mkanda au filamu au kwa njia ya kielektroniki au vinginevyo na inajumuisha ramani, mchoro, picha, filamu, filamu ndogo, mkanda wa video, rekodi ya sauti au rekodi inayosomeka kwa mashine au rekodi yenye uwezo wa kuzalishwa kutoka kwa rekodi inayosomeka kwa mashine kwa njia ya vifaa au programu, au mchanganyiko wa zote mbili, vinavyotumiwa na mkusanyaji kwa madhumuni ya kutunza kumbukumbu; | Tunashauri neon njia na kuwa Taarifa | Neno "taarifa" linaleta mantiki na mtiririko mzuri wa sentensi | "Nyaraka" maana yake ni taarifa yoyote ambayo imerekodiwa, iwe imechapishwa au ipo kwenye mkanda au filamu au kwa njia ya kielektroniki au vinginevyo na inajumuisha ramani, mchoro, picha, filamu, filamu ndogo, mkanda wa video, rekodi ya sauti au rekodi inayosomeka kwa mashine au rekodi yenye uwezo wa kuzalishwa kutoka kwa rekodi inayosomeka kwa mashine kwa njia…." |
| | **Kifungu 3 Tafsiri**<br>"Taarifa binafsi" maana yake ni taarifa kuhusu mtu anayetambulika ambazo zimetunzwa kwa namna yoyote, ikiwa ni pamoja na- (a) taarifa binafsi zinazohusu rangi, asili ya kitaifa au kikabila, dini, umri au hali ya ndoa ya mtu binafsi; (b) taarifa binafsi zinazohusu elimu, historia ya matibabu, ajira au miamala ya kifedha ya mtu binafsi; (c) namba yoyote ya utambulisho, alama au namna nyingine maalum inayomtambulisha mtu binafsi; (d) anwani, alama za vidole au kundi la damu la mtu binafsi; (e) jina la mtu binafsi linaloonekana | Maboresho kuongeza mantiki | 1.Kuongeza neno "anayeweza kutambulika"<br><br>Sababu: mtu anayeweza kutambuliwa mtandaoni.<br><br>2.Kutoa neno jinai Sababu: Jinai ni suala la umma.<br><br>3.Kutoa neno "Miamala ya kifedha" ambalo linahamishiwa kwenye "Taarifa Binafsi Nyeti" | "Taarifa binafsi" maana yake ni taarifa kuhusu mtu anayetambulika au anayeweza kutambulika ambazo zimetunzwa kwa namna yoyote, ikiwa ni pamoja na-<br>(a) taarifa binafsi zinazohusu rangi, asili ya kitaifa au kikabila, dini, umri au hali ya ndoa ya mtu binafsi;<br>(b) taarifa binafsi zinazohusu elimu, historia ya matibabu, jinai, ajira au<br>(c) namba yoyote ya utambulisho, alama au namna nyingine maalum inayomtambulisha mtu binafsi;<br>(d) anwani, alama za vidole au kundi la damu la mtu binafsi; (e) jina la mtu binafsi linaloonekana katika taarifa binafsi za mtu mwingine anayehusiana naye au pale ambapo ufichuzi |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | katika taarifa binafsi za mtu mwingine anayehusiana naye au pale ambapo ufichuzi wa jina hilo utadhihirisha taarifa binafsi za mtu; (f) taarifa iliyotumwa kwa mkusanyaji wa taarifa binafsi na mtu, ambayo ni wazi kuwa taarifa hiyo ni binafsi au ya siri, na majibu kwa taarifa hiyo yanaweza kufichua maudhui ya taarifa ya awali, na mtazamo au maoni ya mtu mwingine yeyote kuhusu mhusika wa taarifa | | | |
| | **Kifungu 3 tafsiri**<br>"Taarifa binafsi nyeti" inajumuisha- (a) taarifa ya vinasaba, taarifa inayohusu watoto, taarifa inayohusu makosa, hukumu za jinai au hatua za kiusalama, taarifa za kibayometriki; (b) ikiwa imechakatwa, ni taarifa binafsi inayoonyesha asili ya rangi au kabila, itikadi za kisiasa, imani za kidini au kifalsafa, ushirika, uanachama wa vyama vya wafanyakazi, jinsia na taarifa za kiafya au mahusiano ya kingono; na (c) taarifa binafsi yoyote ambayo kwa mujibu wa sheria za nchi inachukuliwa kuwa ina athari kubwa kwa haki na maslahi ya mhusika wa taarifa; | Kuongeza "miamala ya kifedha ya mtu binafsi"; | 1. Maelezo zaidi kuhusu 'taarifa inayohusu watoto' ili kuondoa mkanganyiko.<br>2. Maneno "hukumu za jinai" yaondolewe kwenye kundi la taarifa nyeti kwa kuwa ni taarifa zinazopaswa kuwa za umma.<br>3. Kuongeza maneno "taarifa zinazowafanya watoto watambulike"<br>4. Kuondoa kifungu (c) kwa kuwa hakielezi athari zilizotajwa ni zipi, pia kifungu hicho | "taarifa binafsi nyeti" inajumuisha-<br>(a) taarifa ya vinasaba, taarifa inayohusu watoto zinazofanya watoto watambulike, taarifa za kiusalama, taarifa za kibayometriki;<br>(b) ikiwa imechakatwa, ni taarifa binafsi inayoonyesha asili ya rangi au kabila, itikadi za kisiasa, imani za kidini au kifalsafa, jinsia na taarifa za kiafya au mahusiano ya kingono; na<br>(c) miamala ya kifedha ya mtu binafsi; |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | | | kinaweka mamlaka makubwa sana | |
| | **Kifungu 3 tafsiri** "Tume" maana yake ni Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 6; | Kuongeza neno Faragha | Neno faragha linakosekana | "Tume" maana yake ni Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Faragha iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 6; |
| | **Kifungu 3 tafsiri** "Uchakataji" maana yake ni uchambuzi wa taarifa binafsi, kwa njia za kiotomatiki au vinginevyo, kama vile kukusanya, kurekodi au kushikilia taarifa binafsi au kufanya uchambuzi kwenye taarifa binafsi, ikiwa ni pamoja na- (a) kuzipanga upya, kuzichukua na kuzitumia kama zilivyo au kuzibadilisha; (b) kuzirejesha au kuzitumia; au (c) kuziwianisha, kuzichanganya, kuzuia matumizi yake, kuzifuta au kuziharibu; | Kutanua wigo wa neon uchakataji | Kuongeza maneno ~~"Kuzihifadhi" na~~ "kuzisambaza" | "Uchakataji" maana yake ni uchambuzi wa taarifa binafsi, kwa njia za kiotomatiki au vinginevyo, kama vile kukusanya, kurekodi au kushikilia taarifa binafsi au kufanya uchambuzi kwenye taarifa binafsi, ikiwa ni pamoja na-<br>(a) kuzipanga upya, kuzichukua na kuzitumia kama zilivyo au kuzibadilisha;<br>(b) kuzirejesha au kuzitumia; au<br>(c) kuziwianisha, kuzichanganya, kuzuia matumizi yake, kuzifuta au kuziharibu;<br>-(e) kuzisambaza |
| | **Kifungu 3 tafsiri** "Usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi" maana yake ni usafirishaji wowote wa taarifa binafsi wa kimataifa, unaovuka mipaka kwa njia za kielektroniki; na | Kutambua njia mbadala za usafirishaji wa Taarifa | Kuongeza maneno "njia za kawaida" | "Usafirishaji wa taarifa binafsi kwenda nje ya nchi" maana yake ni usafirishaji wowote wa taarifa binafsi wa kimataifa, unaovuka mipaka kwa njia za kielektroniki au njia za kawaida (nyinginezo zozote au nyaraka ngumu) |
| | **Kifungu 3 tafsiri** "Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mawasiliano. | Tunatambua wizara yenye dhamana inaweza kubadilika. Hii inaepusha sheria kutofanyiwa mabadiliko yasiyo ya lazima | Tunatambua wizara yenye dhamana inaweza kubadilika. Hii inaepusha sheria kutofanyiwa mabadiliko yasiyo ya lazima | "Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya kusiamamia sheria hii. |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | **Kifungu cha 4 Malengo ya Sheria**<br>Malengo ya Sheria hii ni-<br>(a) kudhibiti uchakataji wa taarifa binafsi;<br>(b) kuhakikisha kwamba uchakataji wa taarifa binafsi za mhusika wa taarifa unaongozwa na misingi iliyowekwa katika Sheria hii;<br>(c) kulinda faragha za watu binafsi;<br>(d) kuweka utaratibu wa kisheria na kitaasisi wa kulinda taarifa binafsi; na<br>(e) kuwapa wahusika wa taarifa haki na nafuu katika kulinda taarifa binafsi kutokana na uchakataji usiofuata masharti ya Sheria hii. | Maboresho kuweka malengo vizuri zaidi | Tunaamini (b) inaweka msingi, kisha (a) (inavyosomeka kwa sasa) inajazia uzito.<br><br>Katika kifungu kidogo (c) tumeongeza "taarifa binafsi" kwani kimsingi ni sehemu ya malengo mahsusi ya Sheria hii.<br><br>Tumeongeza (f) na (g) kwakuwa ni malengo makubwa zaidi yanayoipa nguvu sheria hii na kusomeka eneo la Malengo ya Sheria ni sehemu sahihi | Tunapendekeza kifungu (a) kuwa (b), na kifungu (b) kuwa (a).<br>1. Malengo yasomeke kama ifuatavyo<br>(a) Kuweka mifumo ya kisheria uitakayohakikisha haki ya faragha na ulinzi wa taarifa binafsi zinalindwa kwa mujibu wa Katiba ya JMT.<br>(b) Kuweka miongozo ya kisheria ya namna ya kukusanya, kuchakata na kudhibiti taarifa binafsi kwa kuzingatia misingi ya viwango vya Kimataifa.<br>(c) Kulinda faragha na taarifa binafsi za watu.<br>(d) Kuweka utaratibu wa kisheria juu ya haki za wahusika wa taarifa binafsi na wajibu wa wakusanyaji, wachakataji na wadhibiti wa taarifa binafsi.<br>(e) kuwapa wahusika wa taarifa haki na nafuu katika kulinda taarifa binafsi kutokana ukusanyaji, uchakataji na udhibiti usiofuata masharti ya Sheria hii.<br>(f) Kuanzishwa kwa mamlaka ya kukuza na kusimamia utekelezaji wa sheria hii.<br>(g) Kusimamia usambazaji wa taarifa binafsi zinazovuka mipaka ya nchi. |
| | **Kifungu cha 5 Misingi ya ulinzi wa taarifa Binafsi**<br>5. Mkusanyaji au mchakataji atahakikisha kwamba taarifa binafsi-<br>(a) zinachakatwa kihalali, kwa haki na kwa uwazi; | Tafsiri haijatambua mdhibiti pamoja na kitendo cha kukusanya na kudhibiti kama inavyoonekana katika kipengele (a) | Tunashari mdhibiti anatakiwa kuguswa na kifungu hiki<br><br>1.Tumeongeza maneno "bila kuingilia haki na faragha za mhusika wa taarifa" kwenye kipengele (a) | 5. Mkusanyaji au mchakataji au mdhibiti atahakikisha kwamba taarifa binafsi<br>(a) zinakusanywa, zinachakatwa na zinadhibitiwa kihalali, kwa haki na kwa uwazi bila kuingilia haki na faragha za mhusika wa taarifa |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | **SEHEMU YA PILI TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI NA FARAGHA** | | |
| | **Kifungu cha 6. Uanzishwaji wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi**<br>-(1) Inaanzishwa Tume itakayojulikana kama Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.<br><br>(2) Tume itakuwa taasisi nafsi yenye mamlaka ya urithishaji wa kudumu na lakiri yake, na kwa jina lake itakuwa na uwezo wa-<br>(a) kumiliki mali zinazohamishika na zisizohamishika, kutoa mali na kuingia mikataba au makubaliano mengine yoyote;<br>(b) kushtaki au kushtakiwa; na (c) kutekeleza jukumu lolote lingine ambalo taasisi nafsi yoyote kisheria inaweza kutekeleza kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu yake chini ya Sheria hii. | (1) Kuongeza neno “FARAGHA”<br><br>Tumependekeza kuongeza kifungu 6(3) | (2) Kuipa uhuru Tume ili isiingiliwe wakati wa utekelezaji wa majukumu yake<br><br>Tumependekeza kuongeza kifungu 6(3) ili kusisitiza uhuru wa tume wakati wa utekelezaji majukumu yake | 6(1) “Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na Faragha<br>(2) Tume itakuwa taasisi nafsi, huru yenye mamlaka ya urithishaji wa kudumu na lakiri yake, na kwa jina lake itakuwa na uwezo wa-<br><br>……..” Kiongezwe kifungu 6(3) na isomeke kama ifuatavyo;<br><br>“Tume itafanya kazi kwa uhuru bila upendeleo wala kuingiliwa katika majukumu yake chini ya Sheria hii”. |
| | **Kifungu cha 7 Majukumu ya Tume**<br>Majukumu ya Tume yatakuwa-<br>(a)kufuatilia utekelezaji wa Sheria hii kwa wakusanyaji;<br>(b)kusajili wakusanyaji na wachakataji kwa mujibu wa Sheria hii; | Tume itoe mwongozo au kanuni, ambazo kwa kutoa notice, itaelekeze aina ya wakusanyaji na wachakataji wanaopaswa kujisajili | Kila mkusanyaji na mchakataji akijisajili utaratibu utachukua muda na kuleta usumbufu kwenye shuguli za kila siku za baadhi ya biashara – hivyo tunapendekeza utekelezaji usiwe wa | S. 7 Tume itasajili wakusanya na wachakataji kwa kutoa notice itakayoonyesha orodha ya wakusanyaji na wachakataji pamoja na taratibu za kufuata ili kujisajili<br><br>Mfano: Kenya kuna vigezo vya usajili chini ya S. 18 ya kuna vigezo kuzingatiwa- aina ya biashara, wingi wa Taarifa zinazochakatuliwa, aina ya Taarifa inayochakatuliwa |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | (c) kupokea, kuchunguza na kushughulikia malalamiko kuhusu madai ya ukiukwaji wa ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu; | | kulazimisha kila mtu kujisajili | Tunashauri uakisi wa S. 18 ya sheria ya Kenya ya Ulinzi wa Taarifa itumike kutoa muongozo ziada – nakala imeambatanishwa. |
| | (d) kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya jambo lolote ambalo Tume itaona linaathiri ulinzi wa taarifa binafsi na faragha za watu;<br><br>(e) kutoa elimu kwa umma kwa kadri itakavyofaa kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii;<br><br>(f) kufanya tafiti na kufuatilia maendeleo ya teknolojia kuhusiana na uchakataji wa taarifa;<br><br>(g) kuanzisha utaratibu wa ushirikiano na mamlaka za nchi nyingine zinazosimamia ulinzi wa taarifa binafsi na kuishauri Serikali katika masuala mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa Sheria hii; na (h) kutekeleza majukumu mengine ya Tume kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii. | Kuongeza upana wa majukumu ya tume | Majukumu ya Tume yasiegemee tu kwa wakusanyaji yaende hadi kwa wachakataji na wadhibiti.<br><br>**PIA**<br>(b) Tunapenekeza kifungu kisilenge USAJILI bali utunzaji wa Orodha ya wakusanyaji, wachakataji na wadhibiti wa Taarifa Binafsi<br><br>Kifungu kidogo (f) tunapendekeza ifanyiwe marekebisho ili iende zaidi ya uchakataji | Majukumu ya Tume yatakuwa-<br>(a)kufuatilia utekelezaji wa Sheria hii kwa wakusanyaji, wachakati na wadhibiti;<br>(b) Kutunza orodha ya kusajili wakusanyaji, wachakataji na wadhibiti kwa mujibu wa Sheria hii;<br>(f) kufanya tafiti na kufuatilia maendeleo ya teknolojia kuhusiana na ukusanyaji, uchakataji, udhibiti na ulinzi wa taarifa; |
| | **Kifungu cha 8 Uanzishwaji wa Bodi**<br><br>8.-(1) Inaanzishwa Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ambayo | | Endapo kifungu hiki kitabakia, tunapendekeza kifanyiwe marekebisho tuliyobainisha kwakuwa: | 1. Kupendekeza na Kuweka kifungu kipya cha (6) Uteuzi wa wajumbe wa Bodi utazingatia usawa wa kijinsia. |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | itakuwa ni chombo cha usimamizi wa Tume na ambacho kitakuwa na wajumbe saba kama ifuatavyo: (a) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti; na (b) wajumbe wengine watano.<br><br>(2) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watateuliwa na Rais kwa kuzingatia utaratibu kwamba iwapo Mwenyekiti anatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Makamu Mwenyekiti atatoka upande mwingine wa Jamhuri ya Muungano.<br><br>(3) Wajumbe wengine watano chini ya kifungu kidogo cha (1)(b) watateuliwa na Waziri kutoka miongoni mwa watu wenye sifa na uzoefu katika eneo la TEHAMA, sheria, uhandisi, fedha au utawala. | | 1. Suala la kuzingatia usawa wa kijinsia halipo kwenye Muswada<br>2. Kifungu 8(3) tunapendekeza muundo huu wa wajumbe wa Bodi | 2.Kurekebisha kifungu cha 8(3) kisomeke; "wajumbe wengine watano (5) chini ya kifungu 1(b) watakuwa kama ifuatavyo;<br>a) Mwakilishi kutoka ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.<br>b) Mjumbe atakayechaguliwa kutoka makampuni ya mawasiliano ya simu.<br>c) Mwakilishi kutoka Tanzania Bankers Association.<br>d) Mwakilishi kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS).<br>e) Mwakilishi kutoka umoja wa watoa huduma ya mtandao (ISP)<br>f) Mwakilishi wa wabunifu wa digiti |
| | **Kifungu cha 11 Mkurugenzi Mkuu**<br>11.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ambaye atateuliwa na Rais. (2) Mtu atateuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa ana sifa zifuatazo: (a) amehitimu katika chuo kikuu kinachotambulika na ana angalau shahada ya kwanza katika nyanja za TEHAMA, uhandisi, sheria, uchumi, fedha au utawala; (b) ana uzoefu wa utumishi usiopungua miaka | Tunapendekeza uwazi na ushindani wa jinsi ya kupata Mkurugenzi wa Tume. | Tunapendekeza uwazi na ushindani wa jinsi ya kupata Mkurugenzi wa Tume ili aweze kufanya kazi za Tume kwa uhuru unaotakikana. | 11.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ambaye ataajiriwa na Bodi kwa njia za uwazi na ushindani.<br>(2) Mtu ataajiriwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa ana sifa zifuatazo:<br>(a) amehitimu katika chuo kikuu kinachotambulika na ana angalau shahada ya kwanza katika nyanja za TEHAMA, uhandisi, sheria, uchumi, fedha au utawala;<br>(b) ana uzoefu wa utumishi usiopungua miaka kumi katika angalau moja ya nyanja zilizotajwa katika aya |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | kumi katika angalau moja ya nyanja zilizotajwa katika aya (a); na (c) ana ujuzi au utaalamu katika nyanja ya ulinzi wa taarifa. | | | (a); na (c) ana ujuzi au utaalamu katika nyanja ya ulinzi wa taarifa.<br>(3) Mchakato wa kumuajiri Mkurugenzi Mkuu wa Tume utakuwa kama ifuatavyo;<br>(a) Bodi itatangaza nafasi ya Mkurugenzi Mkuu kwa umma.<br>(b) Bodi itapokea maombi ya waombaji na kufanya mchujo wa waombaji na kutangaza kwa umma majina ya waombaji waliyofanikiwa katika hatua ya mchujo.<br>(c) Bodi itafanya usaili kwa njia za uwazi na kuteua waombaji watatu (3) waliyofanikiwa katika hatua ya usaili.<br>(d) Bodi itawasilisha majina hayo kwa Rais kwa ajili ya uteuzi.<br>(e) Rais atateua jina la mtu mmoja litakaloidhinishwa na Bunge JMT. |
| | **Kifungu cha 12 Muda wa Kuhudumu wa Mkurugenzi Mkuu**<br>Mkurugenzi Mkuu atashika madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na baada ya kipindi hicho kumalizika, anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja. | | Tunapendekeza kipindi kimoja tu cha Mkurugenzi ili kuhakikisha uhuru wa Mkurugenzi katika kufanya majukumu yake bila kuwaza kuondolewa au kuongezewa kipindi cha uongozi. | Mkurugenzi Mkuu atashika madaraka kwa kipindi kimoja cha miaka sita (6).<br><br>Endapo kuna ulazima wa kurudia office, iwe miaka mitatu, na kurudia miaka mitatu (ukomo uwe miaka 6) |
| | **Kuweka kifungu kipya cha 13** - Ukomo wa Mkurugenzi Mkuu | pendekezo ya kifungu kipya ambacho hakikuwa kwenye Muswada ili kuonesha ukomo wa Mkurugenzi Mkuu. | Mapendekezo ya kifungu kipya ambacho hakikuwa kwenye Muswada ili kuonesha ukomo wa Mkurugenzi Mkuu. | Mkurugenzi Mkuu atakoma kushika wadhifa huo endepo moja kati ya haya yatatokea;<br>a) kupoteza uwezo wa kutekeleza majukumu yake kutokana na ugonjwa wa mwili au akili.<br>b) tabia mbaya au utovu wa nidhamu kwa namna ambayo italeta au kuwa na uwezekano wa kuleta sifa mbaya kwa Tume; |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | | | | c) Ikiwa ametiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai.<br>d) Ikiwa ametangazwa kuwa amefilisika.<br>e) Kifo<br>f) Kujiuzulu |
| | **Kuweka Kifungu kipya 14 -** Utaratibu wa kujaza nafasi ya Mkurugenzi Mkuu | Nyongeza ya kifungu kipya nayopendekezwa | | Iwapo nafasi ya Mkurugenzi Mkuu itatangazwa kuwa wazi, masharti ya kifungu cha 13 yatafuatwa. |
| | **Kupangilia upya vifungu** | Kurudisha mpangilio wa vifungu baada ya mabadiliko | | Hivyo basi, kifungu cha 13 cha Muswada kitakuwa cha 15, cha 14 kitakuwa cha 16 na kuendelea. |
| **SEHEMU YA TATU - USAJILI WA WAKUSANYAJI NA WACHAKATAJI WA TAARIFA BINAFSI** | | | | |
| | | | | |
| | Kifungu . 14. Usajili wa wakusanyaji na Wachakataji<br>14.-(1) Mtu hatakusanya au kuchakata taarifa Binafsi bila kusajiliwa kama mkusanyaji au mchakataji chini ya Sheria hii.<br>(2) Mtu anayekusudia kukusanya au kuchakata Taarifa atawasilisha maombi ya usajili kwa Tume.<br>(3) Tume inaweza, katika muda utakaoainishwa katika kanuni, kukubali au kukataa maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2).<br>(4) Tume itatoa cheti cha usajili kwa mkusanyaji au mchakataji aliyekidhi matakwa ya usajili na kusajiliwa chini ya kifungu hiki. | Sheria itoe haki ya muombaji ambae usajili wake umekatiliwa kurekebisha kosa katika maombi yake ya usajili<br><br>Endapo yote hayo yatashindikanika, sheria itoe haki ya rufaa na iwepo katika sheria kuu na sio kanuni. | Pendekezo la kupata nafasi ya kurekebisha linatokaka na utendaji wa baadhi ya taasisi ambazo bila kukusanya/kuchakata taarifa zitakufa kibiashara.<br><br>Pia haki ya kukataa rufaa ni haki ya kimsingi katika katiba na sheria zetu, hivyo hata hapa kwa kua haki ya msingi itaguswa, haki ya rufaa ni muhimu apatiwe. | S. 14. Usajili wa wakusanyaji na Wachakataji<br>14.-(1) Mtu hatakusanya au kuchakata taarifa Binafsi bila kusajiliwa kama mkusanyaji au mchakataji chini ya Sheria hii.<br>(2) Mtu anayekusudia kukusanya au kuchakata Taarifa atawasilisha maombi ya usajili kwa Tume.<br>(3) Tume inaweza, katika muda utakaoainishwa katika kanuni, kukubali au kukataa maombi yaliyowasilishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2).<br>(4) Tume itatoa cheti cha usajili kwa mkusanyaji au mchakataji aliyekidhi matakwa ya usajili na kusajiliwa chini ya kifungu hiki.<br>(5) Endapo Tume itakataa maombi ya usajili itapaswa<br>kumtaarifu mwombaji kwa maandishi juu ya uamuzi wake na sababu ya uamuzi huo.<br><br>Masharti ya kukubaliwa usajili – |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | (5) Endapo Tume itakataa maombi ya usajili itapaswa kumtaarifu mwombaji kwa maandishi juu ya uamuzi wake na sababu ya uamuzi huo. | | | 6.) Mwombaji atakua na haki ya kurekembisha mapungufu yaliyo katika sababu zilizotolewa na tume ndani ya siku 30<br>7) mkusanyaji au mchakataji ambaye hatakua ameridhishwa na sababu zilizotolewa katika kifungu (5) juu, atatakata rufaa |
| | | Kuweka usajili wa Makundi maalum | Kupunguza mzigo wa majukumu kwa tume | Kifungu 14. (1) kisomeke: “Mara baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, taasisi za nafsi zilizoundwa kisheria na zinazoshughulika na ukusanyaji na uchakataji wa taarifa binafsi zitachukuliwa kuwa zimesajiliwa chini ya Sheria hii na zitapaswa kuzingatia masharti ya Sheria”.<br><br>Taasisi nyingine zitakazo sajiliwa baada ya kutungwa kwa sheria hii zitafuata taratibu za maombi kama kwa mujibu wa kifungu 14 |
| | **Kifungu cha 16 Kipindi cha usajili**<br>16.-(1) Kipindi cha usajili kitakuwa ni miaka mitano kuanzia tarehe ya kutolewa kwa cheti cha usajili.<br>(2) Maombi ya kuhuisha usajili yatawasilishwa ndani ya kipindi cha miezi mitatu kabla ya tarehe ya kuisha kwa kipindi cha usajili kama itakavyoainishwa katika kanuni. | Maboresho na nyongeza ya vifungu | | Tunapendekeza kuondoa kifungu cha 16 (1) na kuweka kifungu kipya 16 (1) ili kuwepo kwa usajili wa kudumu<br><br>Kifungu cha 16 (2) kianzishe ada ya kuhuisha leseni ya wakusanyaji na wachakataji taarifa kila baada ya miaka 3.<br><br>Kifungu cha 16 (2) kilichopo kwenye muswada kiwe cha 16 (3) na kisomeke:<br><br>Maombi ya kuhuisha leseni yatawasilishwa ndani ya kipindi cha miezi mitatu kabla ya tarehe ya kuisha kwa kipindi |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | | | | cha usajili kama itakavyoainishwa katika kanuni.<br><br>Tunapendekeza kuongeza kifungu 16 (4) ili kiweke muda kwa Tume kutoa leseni angalau ndani ya siku 7 za kazi baada ya maombi. |
| | **S. 18 Kufutwa kwa usajili**<br><br>18. Tume inaweza kufuta usajili uliofanyika chini ya Sheria hii kwa utaratibu utakaoainishwa katika kanuni. | Kama kulivyo na vigezo vya usajili, tunashauri viwepo vigezo vya kufuta usajili pia, Tunashauri vigezo hivi viwekwe wazi na kwenye sheria mama ili viweze kumuongoza Waziri/na tume katika utendaji<br><br>Pia tunashauri utaratibu wa kufuata wakati wa ufutaji wa usajili uwekwe wazi kwenye sheria<br><br>Katika ushauri mwingine, Mamlaka ya kufuta usajili yaondolewe, | Kupunguza Nguvu ya tume ili iweze kuongozwa na sheria<br><br>Kuwapa haki wasajiliwa chini ya sheria hii<br><br>Kuwepo kwa utaratibu wa kufuata katika kufuta usalijili<br><br>Kuhakisha ufutaji unafanyika kwa utaratibu maalumu kuzingatia haki na msingi na sio kwa utashi au maamuzi ya mtu mmoja au tume<br><br>Kupunguza rufaa ambazo kupitia kifungu cha 20 zingeenda kwa waziri | 1. Tunapendekeza Vigezo au sababu zitakazo sababisha mtu kufutwa ziwekwe wazi katika sheria hii<br>2. Utaratibu wa ufutaji uwekwe wazi pia – ambapo – pendekezo letu ni kwamba,<br>a. Kuwepo na notisi ya siku 30 ya dhamira ya kutaka kufuta – notisi hiyo ioneshe ni namna gani aliyesajiliwa kakiuka masharti ya sheria hii na kwamba tume inatumia kifungu gani/sababu gani kati ya zitakazoainishwa kwenye kipengele 1 hapo juu<br>b. Aliyesajiliwa apate muda wa kujibu notisi hiyo<br>c. Aliyesajiliwa apate wasaa wa kurekebisha mambo yaliyo orodheshwa katika notisi<br>3. Tume isipewe mamlaka ya kufuta usajili wa taasisi iliyosajiliwa kwa sheria nyingine. Kama kifungu hich kinabaki, basi kifanyiwe marekebisho kuepusha kuua taasisi zilizosajiliwa chini ya sheria nyingine e.g. NIDA |
| | **Kifungu cha 19 Makosa yanayohusiana na usajili**<br>19. Mtu atakayekiuka masharti ya Sehemu hii au kutoa taarifa za uongo | | Kuondoa neno ‘usajili’ na kuweka neno ‘uhuishaji’ | Kisomeke:<br>19. Mtu atakayekiuka masharti ya Sehemu hii au kutoa taarifa za uongo au za kupotosha wakati wa uhuishaji anatenda kosa na endapo atatiwa hatiani |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | au za kupotosha wakati wa usajili au uhuishaji anatenda kosa na endapo atatiwa hatiani atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika kifungu cha 63. | | | atawajibika kwa adhabu iliyoainishwa katika kifungu cha 63 |
| | **Kifungu 20 Rufaa kuhusiana na usajili** 20. Mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wa Tume chini ya Sehemu hii anaweza kuwasilisha rufaa kwa njia ya maandishi kwa Waziri. | Kufutwa kwa kifungu cha 20 | Hakuna haja ya kuwa na kifungu hiki kwa kuwa taasisi hizo zinaweza kuwa zimesajiliwa kwa sheria nyingine. Kama kinabaki, basi kifanyiwe marekebisho kuepusha kuua taasisi zilizosajiliwa chini ya sheria nyingine. Aidha, kukata rufaa kwa Waziri wakati kuna Bodi (endapo itabaki) si mfumo sahihi<br><br>Na kama taasisi hizo hazitaweza kufutwa, sheria itakua inaweka ubaguzi kati ya taasisi nafsi na taasisi za uma | Kuzingatia ushauri wa kufutwa chini ya kifungu no18 na kuepusha ubaguzi kati ya taasisi nafsi na zile za serikali tunashauri kifungu hichi kifutwe na maboresho chini ya kifungu 18 yazingatiwe kwa kipengele a-c |
| | **Kifungu cha 23Chanzo na utoaji wa Taarifa Binafsi**<br><br>S. 23. 23.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), mkusanyaji atakusanya taarifa binafsi moja kwa moja kutoka kwa mhusika wa taarifa. | Kutambua vyanzo vingine vya Taarifa Binafsi<br><br>Kutoa tafsiri ya maneno – eg. wekwa wazi; | Kuna Vyanzo vingine vya Taarifa Binafsi ambavyo ni muhimu kuvitambua mfano:<br>uchukuzi wa Taarifa Binafsi toka Brela, NIDA | S. 23. 23.-(1) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3), mkusanyaji atakusanya taarifa binafsi moja kwa moja kutoka kwa mhusika wa Taarifa au kutokana na vyanzo vingine halali kwa ridhaa ya mhusika au kwa kutimiza matakwa ya sheria. |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | **Kifungu 24 Taarifa Binafsi kutumika kwa Usahihi**<br>24. Kwa kuzingatia madhumuni ambayo taarifa Binafsi zinapendekezwa kutumika, mkusanyaji ambaye ana Taarifa binafsi hatatumia taarifa hizo kwa mazingira yaliyopo bila kuchukua hatua zinazohakikisha kuwa taarifa hizo zimekamilika, ziko sahihi, zinaendana na maudhui na hazipotoshi. | Endapo kifungu hiki kitabaki, basi tunaomba sheria iainishe namna ambayo usahihi wa Taarifa utakavyofanyika<br><br>Taarifa kukamilika itafsiriwe ili kuhakikisha utekelezaji wake kwa ufasaha | Ni vigumu kutimiza matakwa ya sheria pale taarifa zimekusanywa chini ya kifungu 23.3<br><br>Na pia Taarifa zinazokusanya kwa kifungu 23.3 ni vigumu kuhakikisha usahihi wake na kwamba hazitapotosha.<br><br>Masharti ya sheria yasiwe magumu kufanya utelezaji wake kuwa mgumu. | 1. Kifungu hiki kitolewe kwa ugumu wa utekelezaji wake haswa pale Taarifa imekusanywa chini ya kifungu namba 23.3 .<br>2. Tunashauri sheria iainishe namna utekelezaji huu utafanyika<br>3. Maana/tafsiri ya Taarifa kukamilika pia itolewe kwenye sheria – ili utekelezaji wake uweze kutimia<br><br>Maboresho mbadala<br>24. Kwa kuzingatia madhumuni ambayo taarifa Binafsi zinapendekezwa kutumika, mkusanyaji ambaye ana Taarifa binafsi hatatumia taarifa hizo kwa mazingira yaliyopo bila kuchukua hatua zinazohakikisha kuwa taarifa hizo zimechukuliwa kwa usahihi. ~~zimekamilika, ziko sahihi, zinaendana na maudhui na hazipotoshi.~~ |
| | **Kifungu cha 27 usalama wa Taarifa binafsi**<br>(1) Mkusanyaji na wawakilishi wake watahakikisha kuwa taarifa binafsi zinalindwa, kwa kuchukua hatua za kiusalama zinazohitajika kwa usalama wa taarifa hizo dhidi ya upotevu wa kizembe, uteketezaji, ubadilishaji, upatikanaji au uchakataji wa taarifa binafsi bila idhini. | Kuongeza wigo wa uwajibikaji | Neno "mchakataji" liongezeke kwenye 27(1) ili kutoweka mianya yoyote | Mkusanyaji, Mchakataji na wawakilishi wao watahakikisha kuwa taarifa binafsi zinalindwa, kwa kuchukua hatua za kiusalama zinazohitajika kwa usalama wa taarifa hizo dhidi ya upotevu wa kizembe, uteketezaji, ubadilishaji, upatikanaji au uchakataji wa taarifa binafsi bila idhini. |
| | **Kifungu cha 28 Uhifadhi na utoaji wa Taarifa binafsi** | Tunashauri namna Taarifa itakavyohifadhiwaiw | Technolojia hubadilika haraka na njia mpya na bei nafuu hujitokeza, | Uhifadhi na utoaji wa Taarifa binafsi<br>28.-(1) Endapo mkusanyaji atatumia taarifa binafsi kwa |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | 28.-(1) Endapo mkusanyaji atatumia taarifa binafsi kwa madhumuni maalum kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 25, atatakiwa kuhifadhi taarifa hizo kwa kipindi ambacho kitaainishwa katika kanuni ili kuhakikisha kuwa mhusika wa taarifa anapata fursa ya kuzipata taarifa hizo pale atakapozihitaji.<br>(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza, kwa kanuni, kuanisha taratibu za uhifadhi na uteketezaji wa taarifa binafsi alizonazo mkusanyaji kwa kuzingatia madhumuni ya uhifadhi. | ekwe wazi ili kuwapa wakusanyaji au wachakataji uhuru wa kuhifadhi Taarifa kwa bei nafuu na kuendana na matumizi ya kisasa | Taarifa huchakataliwa kwa urahisi pale Taarifa zimehifadhiwa ki-electronic<br><br>Na pia mifumo mingi ya ki-uchambuzi inatumia cloud technology kuleta ufanisi zZaidi katika uchakataji | madhumuni maalum kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 25, atatakiwa kuhifadhi taarifa hizo kwa kipindi kilichoainisha katika sheria zilizopo au kwa kipindi ambacho kitaainishwa katika kanuni ili kuhakikisha kuwa mhusika wa taarifa anapata fursa ya kuzipata taarifa hizo pale atakapozihitaji.<br>(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1), Waziri anaweza, kwa kanuni, kuanisha taratibu za uhifadhi na uteketezaji wa taarifa binafsi alizonazo mkusanyaji kwa kuzingatia madhumuni ya uhifadhi.<br>1. Uhifadhi wa Taarifa unaweza kufanywa kielectroniki au katika namna ambayo Taarifa imekusanywa.<br>2. Taarifa Binafsi zinaweza kuhifadhiwa katika njia ya kieletroniki kwa kuzingatia Ulinzi na usalama wa Taarifa hizo. |
| | **Kifungu cha 29 Usahihishaji wa taarifa binafsi**<br>29.-(1) Endapo katika nyaraka au jalada ambalo upatikanaji wake umeruhusiwa chini ya Sheria hii kuna Taarifa binafsi ambazo mhusika wa taarifa hizo anadai kuwa-<br>(a) hazijakamilika, sio sahihi au zinapotosha; au<br>(b) haziendani na dhumuni la uhifadhi wa Taarifa husika, mkusanyaji, kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa katika kanuni, na baada ya kupokea maombi ya mhusika wa taarifa na kujiridhisha nayo, anaweza kurekebisha taarifa hizo. | Mabadiliko haya yaelekezwe kwa mkusanyaji wa kwanza wa Taarifa Binafsi<br><br>Kanuni zitakazo tungwa chini ya kifungu hichi zihusishe wadau wote – wakusanyaji na wachakataji | Mabadiliko yaelekezwe kwa mkusanyaji wa kwanza ili mabadiliko yafuate mkondo wakusanyaji wa pili na wachakataji<br><br>Kanuni zitakazo tungwa chini ya kifungu hichi zihusishe wadau wote – wakusanyaji na wachakataji ili kutoa njia bora na inayotekelezeka ya kufanya mabadiliko ya taarifa | Usahihishaji wa taarifa binafsi<br>29.-(1) Endapo katika nyaraka au jalada ambalo upatikanaji wake umeruhusiwa chini ya Sheria hii kuna Taarifa binafsi ambazo mhusika wa taarifa hizo anadai kuwa-<br>(a) hazijakamilika, sio sahihi au zinapotosha; au<br>(b) haziendani na dhumuni la uhifadhi wa Taarifa husika, mkusanyaji, kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa katika kanuni, na baada ya kupokea maombi ya mhusika wa taarifa na kujiridhisha nayo, anaweza kurekebisha taarifa hizo.<br>(2) Mkusanyaji, wakati wa kufanya marekebisho kwenye taarifa binafsi chini ya kifungu hiki, atahakikisha kuwa hafuti kumbukumbu ya |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | (2) Mkusanyaji, wakati wa kufanya marekebisho kwenye taarifa binafsi chini ya kifungu hiki, atahakikisha kuwa hafuti kumbukumbu ya maandishi ya nyaraka kama ilivyokuwa kabla ya marekebisho.<br>(3) Endapo mkusanyaji hataridhika na sababu za maombi chini ya kifungu kidogo cha (1), anaweza kukataa kufanya marekebisho yoyote kwenye taarifa binafsi na kumtaarifu mwombaji sababu za kukataa maombi. | | | maandishi ya nyaraka kama ilivyokuwa kabla ya marekebisho.<br>(3) Endapo mkusanyaji hataridhika na sababu za maombi chini ya kifungu kidogo cha (1), anaweza kukataa kufanya marekebisho yoyote kwenye taarifa binafsi na kumtaarifu mwombaji sababu za kukataa maombi.<br>4. kanuni na miongozo ya hatua za usahihishaji zitatungwa na tume kwa kushirikiana na wadau.<br>5. notice kwa watumiaji wengine |
| | **Kifungu cha 30 Katazo la uchakataji wa**<br>**taarifa Binafsi nyeti**<br><br>30.-(1) Mtu hatachakata taarifa binafsi nyeti bila ridhaa ya maandishi ya mhusika wa taarifa | Neon *Maandishi* lipatiwe tafsiri pana itakayojumlisha maendeleo ya sayansi na technolojia haswa vile Taarifa nyingi hukusanywa k-electroniki | Kutanua wigo wa tafsiri ya neon maandishi na kujuisha ridhaa ambayo inaweza kupatikanika kwa njia mbadala | 30.-(1) Mtu hatachakata taarifa binafsi nyeti bila ridhaa ya ~~maandishi~~ ya mhusika wa Taarifa ambayo itahifadhiwa kwa maandishi au kielectroniki |
| | **Kifungu cha 30 Katazo la uchakataji wa**<br>**taarifa Binafsi nyeti**<br><br>30(3) (3) Waziri, kupitia kanuni, anaweza kuamua mazingira ambayo katazo la uchakataji wa taarifa binafsi lililoelezwa chini ya kifungu hiki halitaweza kuondelewa hata kwa ridhaa ya mhusika wa taarifa. | Kufutwa kwa kifungu 30(3) | Sheria imeshaainisha mazingira ya uchakataji, na vile mmiliki wa Taarifa atakua ameridhia, sheria inakua imempa Waziri mamlaka makubwa Zaidi ya mmiliki wa taarifa | ~~30 (3) (3) Waziri, kupitia kanuni, anaweza kuamua mazingira ambayo katazo la uchakataji wa taarifa binafsi lililoelezwa chini ya kifungu hiki halitaweza kuondelewa hata kwa ridhaa ya mhusika wa taarifa.~~ |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| | **SEHEMU YA TANO - USAFIRISHAJI WA TAARIFA BINAFSI NJE YA NCHI** | | | |
| | **Kifungu cha 32 Kusafirisha kwenda nchi isiyo na Ulinzi wa kutosha wa taarifa Binafsi**<br>32 (5) ikiwa mkusanyaji ataihakikishia Tume kwamba kuna ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi, uhuru na haki za msingi za mhusika wa taarifa, na utekelezaji wa haki za mhusika wa taarifa, na kwamba ulinzi huo unaweza kutekelezwa kupitia hatua. | | Kuweka urahisi wa kutimiza matakwa na kuweka uwajibikaji kwa wakusananyaji na wachakataji | ikiwa mkusanyaji ~~ataihakikishia Tume~~ atahakikisha kwamba kuna ulinzi wa kutosha wa taarifa binafsi, uhuru na haki za msingi za mhusika wa taarifa, na utekelezaji wa haki za mhusika wa taarifa, na kwamba ulinzi huo unaweza kutekelezwa kupitia hatua. |
| | **SEHEMU YA SITA - HAKI ZA WAHUSIKA WA TAARIFA** | | | |
| | **Kifungu cha 33 Haki ya kupata taarifa binafsi**<br>33.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, mhusika wa taarifa ana haki ya- (a) kufahamishwa na mkusanyaji yeyote endapo taarifa binafsi zinachakatwa na mkusanyaji huyo au mkusanyaji mwingine kwa niaba ya mkusanyaji huyo; | | Sheria hii inatakiwa kuweka kwa wigo mpana Haki za Mhusika wa Taarifa ili kuhakikisha ulinzi wa taarifa zake umezingatiwa zaidi kwa mujibu wa Sheria. | Haki za mhusika wa taarifa binafsi (marginal note)<br>33.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, mhusika wa taarifa ana haki ya-<br>(a) kutaarifiwa namna taarifa zake binafsi zitakavyotumika<br>(b) kupata fursa ya kutazama taarifa binafsi zilizohifadhiwa na mkusanyaji au mchakataji<br>(c) kupinga au kusitisha uchakataji wa baadhi ya taarifa au taarifa zote za kibinafsi<br>(d) kufanya marekebisho ya taarifa binafsi zisizo za kweli au danganyifu<br>(e) kufuta au kuharibu taarifa binafsi za uongo au danganyifu zinazomhusu mhusika wa taarifa binafsi<br><br>33(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), (a), (b), (c), (d) na (e), mkusanyaji au mchakataji hatalazimika kutoa taarifa kwa mhusika wa taarifa endapo taarifa hizo-<br>(a) zinahusika katika uchunguzi kwa mujibu wa sheria. |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | | | | (b) zimezuiliwa kwa amri ya mahakama. |
| | **Kifungu 33 (1) (c)**<br>pale ambapo uchakataji wa taarifa binafsi kwa njia ya kiotomatiki kwa madhumuni ya kutathmini masuala yanayomhusu, umetumika au unaweza kutumika kama msingi pekee wa maamuzi yenye athari kubwa kwake, kufahamishwa na mkusanyaji kuhusu sababu zilizotumika kufikia uamuzi huo.<br><br>33(1) (c) (iii) wapokeaji au makundi ya wapokeaji waliopewa au wanaoweza kupewa taarifa hizo; | Liongezwe neno "ukusanyaji" baada ya maneno pale ambapo…" | Kutanua wigo na kuhusisha wakusanyaji | pale ambapo ukusanyaji, uchakataji wa taarifa binafsi kwa njia ya kiotomatiki kwa madhumuni ya kutathmini masuala yanayomhusu, umetumika au unaweza kutumika kama msingi pekee wa maamuzi yenye athari kubwa kwake, kufahamishwa na mkusanyaji kuhusu sababu zilizotumika kufikia uamuzi huo. |
| | Mhusika wa taarifa, kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa kwenye kanuni, anaweza kumtaka mkusanyaji kuacha kuchakata taarifa zake binafsi kwa madhumuni ya matangazo ya biashara. | Kutanua wigo na kujumlisha mchakataji wa taarifa | | Mhusika wa taarifa, kwa kuzingatia utaratibu utakaoainishwa kwenye kanuni, anaweza kumtaka mkusanyaji au mchakataji kuacha kuchakata taarifa zake binafsi kwa madhumuni ya matangazo ya biashara. |
| | **Kifungu namba 37 Haki ya fidia**<br><br>37.-(1) Mhusika wa taarifa atakayepata madhara kwa sababu za ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii uliofanywa na mkusanyaji atakuwa na haki ya kulipwa fidia kutoka kwa mkusanyaji kutokana na madhara hayo. | •Kifungu cha 37(1) hakijamuhusisha mchakataji kulipa fidia endapo atasababisha madhara kwa mhusika wa taarifa kutokana na kukiuka masharti ya Sheria hii. | | •37.-(1) Mhusika wa taarifa atakayepata madhara kwa sababu za ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii atakuwa na haki ya kulipwa fidia kutokana na madhara hayo.<br><br>•37 (2) Kifungu hiki kifutwe<br><br>•37 (3) Endapo Ofisi ya Mlinzi wa Taarifa Binafsi itajiridhisha na maombi ya mhusika wa taarifa kwamba kuna hatari kubwa ya ukiukwaji Zaidi |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | (2) Mhusika wa taarifa ambaye haki zake zimevunjwa kwa sababu ya ukiukwaji wa masharti yoyote ya Sheria hii atakuwa na haki ya kulipwa fidia kutoka kwa mkusanyaji ikiwa-<br>(a) mlalamikaji ndiye mhusika wa taarifa aliyeathiriwa;<br>(b) haki za mhusika wa taarifa zimevunjwa kwa sababu ya ukiukwaji huo; na<br>(c) athari hizo zinahusiana na uchakataji wa Taarifa binafsi kinyume na masharti ya Sheria hii.<br>(3) Endapo Tume itajiridhisha na maombi ya mhusika wa Taarifa<br>(a) kwamba amepata madhara kwa sababu ya ukiukwaji wa masharti ya Sheria hii uliofanywa na mkusanyaji au mchakataji kuhusiana na taarifa binafsi yoyote, katika mazingira yanayompatia haki ya kulipwa fidia chini ya kifungu hiki; na<br>(b) kwamba kuna hatari kubwa ya ukiukwaji Zaidi kuhusiana na taarifa binafsi husika katika mazingira hayo, Tume inaweza kuamuru kurekebishwa, kuzuiwa, kufutwa au kuharibiwa kwa taarifa hizo.<br>(4) Tume, pale ambapo imetoa amri chini ya kifungu kidogo cha (3) na endapo itaona kuwa ni busara, inaweza | •Kifungu kidogo cha 2 kinarudia yale ambayo yapo kwenye kifungu kidogo cha 1, hivyo tunapendekeza kifutwe.<br>•37 (4) Ofisi isitumie busara ila inapaswa kuamuru wahusika wengine wa taarifa wapewe taarifa.<br>•37 (5) kifungu hiki kinakosa mantiki kwa kuzingatia marekebisho yaliyofanywa kwenye kifungu kidogo cha 4, hivyo tunapendekeza kifungu hiki kifutwe | | kuhusiana na taarifa binafsi husika, Ofisi inaweza kuamuru kurekebishwa, kuzuiwa, kufutwa au kuharibiwa kwa taarifa hizo.<br><br>•37 (4) Ofisi ya Mlinzi wa Taarifa Binafsi, pale ambapo imetoa amri chini ya kifungu kidogo cha (3) inaweza kumuamuru mkusanyaji au mchakataji kuwajulisha wahusika wengine ambao wamepatiwa taarifa binafsi kuhusu marekebisho, zuio, ufutaji au uharibifu wa taarifa hizo. |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | kumuamuru mkusanyaji au mchakataji kuwajulisha wahusika wengine ambao wamepatiwa taarifa binafsi kuhusu marekebisho, zuio, ufutaji au uharibifu wa taarifa hizo.<br>(5) Katika kuamua endapo ni sahihi kuhitaji Taarifa chini ya kifungu kidogo cha (4), Tume itazingatia idadi ya watu ambao watapaswa kuarifiwa. | | | |
| | **Kifungu cha 38 Kurekebisha, kuzuia, kufuta na kuharibu taarifa Binafsi**<br>Kifungu 38 Kurekebisha, kuzuia, kufuta na kuharibu taarifa Binafsi<br><br>38.-(1) Pale ambapo Tume itaridhika kwa maombi ya mhusika wa taarifa kuwa taarifa binafsi zinazomhusu mhusika huyo siyo sahihi, Tume inaweza kumuamuru mkusanyaji au mchakataji kurekebisha, kuzuia, kufuta au kuharibu taarifa hizo | Kifungu hich kifutwe au kiboreshwe | kifungu hiki kinakosa mantiki kwa kuzingatia marekebisho yaliyofanywa kwenye kifungu cha 33 na 37, hivyo tunapendekeza kifungu hiki kifutwe | **Kifungu hiki kiboreshwe na kiandikwe upya kama ifuatavyo;**<br>Kwa kuzingatia sheria za nchi zilizopo, Mhusika wa taarifa au mwakilishi wake wa kisheria kama itakavyokuwa anaweza kumuomba kwa maandishi mkusanyaji au mdhibiti taarifa kufuta taarifa binafsi za mhusika wa taarifa iwapo;<br>a) Mdhibiti taarifa hana mamlaka ya kuendelea kubaki na hizo taarifa.<br>b) Mhusika wa Taarifa hakutoa au ameondoa ridhaa yake.<br>c)Taarifa binafsi hazina uhalisia kwa madhumuni yaliyolengwa.<br>d) taarifa binafsi zimechakatwa au zilikusanywa kinyume cha sheria. |
| | Pendekezo la kuongeza Kifungu kipya cha 38 (3) | Kuweka mda wa mkusanyaji na mchakataji kutelekeza ombi la ufutaji | Kuweka uwajibikaji wa wakati | Kuweka kifungu kipya 38 (2)<br><br>“Baada ya kupokea ombi la kufuta taarifa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), na kwa kuzingatia matakwa ya sheria nyingine za nchi, mdhibiti au mkusanyaji taarifa anawajibu wa kufuta taarifa binafsi ndani ya masaa 48 (siku mbili za kazi) |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | Pendekezo la Kifungu kipya cha 38 (3) | | | Mdhibiti wa taarifa atakuwa na jukumu la kuwataarifu wakusanyaji, wachakataji na mtu mwingine kwamba taarifa binafsi za mtu huyo amewasilisha maombi ya kufuta taarifa zake. |
| | Pendekezo la Kifungu kipya cha 38 (4) | | | Mdhibiti taarifa anaweza asifute taarifa kwa mujibu wa maombi ya kifungu cha 38 (1) kwa ajili ya kufanikisha yafuatayo;<br>a) Utekelezaji wa hukumu ya madai au jinai<br>b) Kwa madhumuni mdhibiti taarifa ya kufuata taratibu za kisheria.<br>c) Kwa maslai ya umma yanayohusiana na afya ya jamii, takwimu, utafiti wa kisayansi na kihistoria ambapo kufutwa kwa taarifa hizo kunaweza kuathiri uchakataji.<br>d) Kwa ajili ya kukuza uhuru wa kupata taarifa na kujieleza kwa mujibu ya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania, 1977.<br>e) Kwa kutimiza masharti ya sheria zingine zinazotaka Taarifa ziendelee kuhifadhiwa au kuchakatuliwa |
| | **SEHEMU YA SABA UCHUNGUZI WA MALALAMIKO** | | | |
| | **Kifungu 39 Malalamiko dhidi ya ukiukwaji wa misingi ya ulinzi wa taarifa**<br>**binafsi**<br><br>39(1)(b) Ukuwasilisha malalamiko | | Uwekwe urahisi wa uwasilishaji malalamiko, wahusika wa taarifa wasikilizwe kwa njia mbalimbali | "Mtu yeyote…………..anaweza kuwasilisha malalamiko kwa njia ya mdomo au kwa maandishi au njia nyingine za kielekitroniki"…. |
| | **Kifungu cha 39 Malalamiko dhidi yaukiukwaji wa misingi ya ulinzi wa Taarifa Binafsi**<br>Kifungu 39 (3) 3) Malalamiko yatakayowasilishwa katika kifungu hiki | Tunapendekeza siku zisiwe 90, bali ziwe 60. | Kupunguza siku za kukamilisha malalamiko | 3)Malalamiko yatakayowasilishwa katika kifungu hiki yatachunguzwa na kumalizika ndani ya siku sitini (60) tangu tarehe ya kupokelewa. |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | yatachunguzwa na kumalizika ndani ya siku tisini tangu tarehe ya kupokelewa | | | |
| | | | | |
| | **Kifungu cha 42 Mamlaka ya Tume wakati wa uchunguzi**<br><br>S. 42(1) (d)Wakati wa kuchunguza malalamiko, tume itakua na mamlaka ya<br><br>(d) – Kumhoji mtu yeyote au kuondoka na kifaa chochote chenye Taarifa Binafsi katika jengo lolote alimoingia kwa mujibu wa mamlaka ya aya C | Kufuta mamlaka ya tume kuondoka na kifaa na kuipa tume haki ya kupata taarifa original (grant access to oringal data or system where that info is stored)<br><br>Ni muhimu kupata kibali cha mahakama cha kuiwezesha tume kuondoka na kifaa chochote | Biashara nyingi zinawezakufa kwa sababu ya tume kuondoka na vifaa ambavyo vitatumika katika kuendesha shughuli za kila siku za taasisi husika<br><br>Itatosha tume ikipata Taarifa original au system access.<br><br>Pia zama hizi wengi hutumia cloud technology, ngumu kutekelezeka<br>Ni muhimu kupata kibali cha mahakama cha kuiwezesha tume kuondoka na kifaa chochote | (d) – Kumhoji mtu yeyote ~~au kuondoka na kifaa chochote chenye Taarifa Binafsi~~ au kupata Taarifa yoyote katika jengo lolote alimoingia kwa mujibu wa mamlaka ya aya C.<br><br>**Pendekezo ziada**<br>(e) Kabla ya kutekeleza majukumu chini ya kifungu D, tume itahakikisha ina kibali cha mahakama chenye kuruhusu utekelezaji huo.<br><br>**Pendekezo mbadala**<br><br>42(1)(f) Kabla ya kutekeleza majukumu yake kama ilivyoainishwa katika aya (c),(d) na (e) ya kifungu kidogo cha 1, Tume inapaswa kuwa na kibali cha mahakama kinachoainisha sababu za kuingia katika jengo, sababu za kuondoka na kifaa au nakala yoyote na viwe vinahusiana na kosa litakalokuwa limeainishwa katika kibali hicho |
| | **Kifungu cha 42 Mamlaka ya Tume wakati wa uchunguzi**<br>Kifungu 42 (e)<br>(e) kuchunguza au kupata nakala za, au dondoo kutoka kwenye vitabu, nyaraka au kumbukumbu nyingine zilizopatikana katika jengo alimoingia | Ni muhimu kupata kibali cha mahakama ili Tume kuweza kuchunguza vitabu, nyaraka au kumbukumbu | Ni muhimu kupata kibali cha mahakama ili Tume kuweza kuchunguza vitabu, nyaraka au kumbukumbu | (e) kuchunguza au kupata nakala za, au dondoo kutoka kwenye vitabu, nyaraka au kumbukumbu nyingine zilizopatikana katika jengo alimoingia kwa mujibu wa aya (c) zenye suala lolote linalohusika na uchunguzi baada ya kupata kibali cha mahakama. |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | kwa mujibu wa aya (c) zenye suala lolote linalohusika na uchunguzi. | | | |
| | S. 42 (2) (2) Wakati wa uchunguzi wa malalamiko chini ya kifungu hiki, mlalamikaji na mkusanyaji anayelalamikiwa anaweza kupewa nafasi ya kufanya mawasilisho kwa Tume. | Mlalamikiwa apewe haki ya kutoa utetezi wake kama haki ya msingi<br><br>Pia mlalamikiwaji na mwenye Taarifa wapewe nafasi ya kusuluhisha migogoro | Haki ya kujilinda na kujitetea/kusikilizwa ni ya kimsingi na mlalamikiwaji apewe nafasi ya kujitetea<br><br>Nafasi ya upatanishi itapunguza garama za upelelezi za tume na kutoa nafasi kwa upatanishi kati ya mwenye data na mlalamikiwa | S. 42 (2) (2) Wakati wa uchunguzi wa malalamiko chini ya kifungu hiki, mlalamikaji na mkusanyaji anayelalamikiwa ~~anaweza kupewa~~ atapewa nafasi ya kufanya suluhisho baina yao na kuwasilisha muafaka wa masuluhisho yao ~~mawasilisho~~ kwa Tume ndani ya siku 30 |
| | Kifungu 42 (3)<br>Bila kujali sheria nyingine yoyote, Tume inaweza kuchunguza taarifa binafsi iliyorekodiwa katika namna yoyote inayohifadhiwa na mkusanyaji, na katika kufanya hivyo, Tume haitazuiliwa kupata taarifa yoyote. | | Hakuna mtu wala chombo kilicho juu ya Sheria, Ibara ya 13 ya Katiba ya JMT. | Kifungu hiki kifutwe, kinaipa Tume mamlaka makubwa ya kutozingatia sheria nyingine za nchi. |
| | **Kifungu 47 Faini za kiutawala**<br>6) Mtu atakayebainika kutenda kosa chini ya kifungu hiki atakapotiwa hatiani atawajibika- (a) ikiwa ni mtu binafsi, kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni ishirini au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi au vyote kwa pamoja; na (b) ikiwa ni kampuni au shirika, kulipa faini isiyopungua shilingi | Kupunguza Kiwango cha adhabu | Kuweka adhabu itakayolipika bila kuadhiri uhai wa taasisi husika | 6) Mtu atakayebainika kutenda kosa chini ya kifungu hiki atakapotiwa hatiani atawajibika- (a) ikiwa ni mtu binafsi, kulipa faini isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi milioni ishirini au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka kumi au vyote kwa pamoja; na (b) ikiwa ni kampuni au shirika, kulipa faini isiyopungua shilingi milioni moja na isiyozidi shilingi milioni 500. |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | milioni moja na isiyozidi shilingi bilioni tano. | | | |
| | **Kifungu 58 Mazingira yanayoondolewa katika mawanda ya Sheria hii**<br>58 (3) (3) Waziri anaweza kuanisha mazingira mengine ambayo yanaweza kuondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii na masharti mengine kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki. | Tunapendekeza kifungu hiki kifutwe | Kifungu hiki hakina uhitaji wa msingi kuwepo kwasababu tayari kifungu kidogo cha 2 kimeainisha mazingira ambayo uchakataji wa taarifa binafsi unaweza kuondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii | ~~(3) Waziri anaweza kuanisha mazingira mengine ambayo yanaweza kuondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii na masharti mengine kuhusu utekelezaji wa kifungu hiki.~~ |
| | **Kifungu cha 60 Makosa ya ufichuaji wa taarifa Binafsi kinyume cha sheria**<br><br>60 (1) (2) Mkusanyaji ambaye, bila sababu za msingi, atafichua taarifa binafsi kwa njia yoyote ambayo haiendani na madhumuni ambayo taarifa hiyo imekusanywa anatenda kosa. | Kuongeza neno mchakataji na mdhibiti. | Kuongeza wigo wa uwajibikaji kwa wadau wengine | 65.-(1) Kila mkusanyaji, mchakataji na mdhibiti atapaswa kutengeneza kanuni za maadili au sera kwa ajili ya ulinzi wa taarifa binafsi zitakazobainisha maadili na miiko inayopaswa kuzingatiwa wakati wa ukusanyaji au uchakataji wa taarifa binafsi. |
| | **Kifungu cha 64 Kanuni**<br>64 (2) Bila kujali ujumla wa kifungu kidogo cha (1), kanuni zitakazotengenezwa chini ya kifungu hiki zinaweza kuainisha-<br>(a) mazingira ambayo yataondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii; | Tunapendekeza kifungu hiki kifutwe. | Kwa kuzingatia mapendekezo ya kifungu cha 58(3) tunapendekeza kifungu hiki kifutwe sababu hakihitajiki tena. | (2) Bila kujali ujumla wa kifungu kidogo cha (1), kanuni zitakazotengenezwa chini ya kifungu hiki zinaweza<br>kuainisha-<br>(a) mazingira ambayo yataondolewa katika mawanda ya masharti ya Sheria hii; |

| S/N | Sehemu katika Mswada unaopendekezwa | Mabadiliko yanayopendekezwa | Sababu za mapaendekezo | Pendekezo la maeno baada ya kuzingatia mabadiliko |
|---|---|---|---|---|
| | **Kifungu cha 65 Kanuni za maadili ya ulinzi wa Taarifa binafsi**<br><br>65.-(1) Kila mkusanyaji atapaswa kutengeneza kanuni za maadili au sera kwa ajili ya ulinzi wa taarifa Binafsi zitakazobainisha maadili na miiko inayopaswa kuzingatiwa<br>wakati wa ukusanyaji au uchakataji wa taarifa binafsi.<br>(2) Kanuni au sera chini ya kifungu kidogo cha (1) zitawasilishwa kwa Tume kwa ajili ya mapitio na kuidhinishwa.<br>(3) Wakati wa mapitio wa kanuni au sera za maadili, Tume itajiridhisha, pamoja na mambo mengine, endapo rasimu za kanuni au sera za maadili zilizowasilishwa zimezingatia<br>masharti ya Sheria hii na ya sekta husika na pale itakapoona inafaa, inaweza kutafuta maoni ya wahusika wa taarifa au wawakilishi wao na kushauriana na mkusanyaji husika kwa madhumuni ya kufanya marekebisho muhimu kabla ya<br>kuziidhinisha. | Sheria au kanuni zitunge kanuni itakayo tumika kama mfano | Lengo ni kuhakikisha misingi mikuu ya sheria hii inazingatiwa katika kanuni hiyo na wadau kuweza kuongezea kutokana na mazingira yao ya biashara | Kanuni za maadili ya ulinzi wa taarifa<br>binafsi<br><br>65.-(1) Kila mkusanyaji atapaswa kutengeneza kanuni za maadili au sera kwa ajili ya ulinzi wa taarifa Binafsi zitakazobainisha maadili na miiko inayopaswa kuzingatiwa wakati wa ukusanyaji au uchakataji wa taarifa binafsi.<br>(2) Kanuni au sera chini ya kifungu kidogo cha (1) zitazingatia misingi kama ilivyoonyeshwa kat jedwali na zitawasilishwa kwa Tume kwa ajili ya mapitio na kuidhinishwa.<br>(3) Wakati wa mapitio wa kanuni au sera za maadili, Tume itajiridhisha, pamoja na mambo mengine, endapo rasimu za kanuni au sera za maadili zilizowasilishwa zimezingatia<br>masharti ya Sheria hii na ya sekta husika na pale itakapoona inafaa, inaweza kutafuta maoni ya wahusika wa taarifa au wawakilishi wao na kushauriana na mkusanyaji husika kwa madhumuni ya kufanya marekebisho muhimu kabla ya<br>kuziidhinisha. |

Alternative Dispute Resolution

40. (1) The provisions of this part shall not preclude the data subject from bringing a complaint directly to the independent dispute resolution mechanism established by a data processor or controller to investigate and resolve Data Subject complaints and to provide appropriate recourse.

(2) Where parties reach an amicable settlement through a mechanism established under subsection (1), the same shall be filed with the Commission within 14 days and the settlement agreement shall be final and conclusive.

(3) Once the settlement agreement is filed pursuant to subsection (2) above, no appeal shall lie in respect thereof.

(4) The data controller or data processor who prefers an independent dispute resolution shall include the relevant information regarding such mechanism in their websites or other widely used mediums. The information required under this subsection shall include, but not limited to, procedures and remedies to be granted.

56. (1) Where a processing is considered evaluable under the provisions of section 55(1) of this Act, a data controller or data processor shall, prior to the processing, and in addition to the conditions imposed by the Commissioner or Deputy Commissioner under section 55 (3), carry out a data protection impact assessment.

Data Protection Impact Assessment

(2) A data protection impact assessment shall comprise the following;

(a) a logical description of the anticipated processing operations and the principles for the processing, including, where relevant, the lawful interest pursued by the data controller;

(b) an evaluation of the inevitability and proportionality of the processing operations in relation to the purposes;

(c) an evaluation of the privacy risks to the data subjects;

(d) the contemplated prevention and mitigation measures for addressing privacy risks and the safeguards to ensure the protection of personal data and to establish compliance with this Act, in consideration of the rights, and lawful interests of data subjects and other persons concerned.

(3) The data controller or data processor shall consult the Commissioner or Deputy Commissioner prior to the processing of such data in the event where a data protection impact assessment prepared under this section points out that such data processing would result in a high risk to the rights and freedoms of a data subject concerned.

(4) For the purposes of this section, a "data protection impact assessment" means an evaluation of the impact of the contemplated processing operations on the rights of data subject and security of personal data.

(5) The data impact assessment reports shall be submitted forty days prior to the processing of data.

(6) The Commissioner or Deputy Commissioner shall set out guidelines for carrying out an impact assessment under this section.

33. (1) A data subject or his personal legal representative as the case may be, may request a data controller to; Right to be Forgotten

(a) Completely erase personal data about the data subject where;

(i) the data controller no longer has the authority to retain such personal data;

(ii) data subject withdraws consent;

(iii) the personal data is no longer relevant for purpose for which it was collected; or

(iv) where the personal data is processed or were obtained unlawfully.

(2) Upon receipt of the request under subsection (1), a data controller has an obligation to completely erase personal data without undue delay.

(3) It shall be an obligation of the data controller to inform each data processor and / or third party to whom disclosure of the erased personal data was made that the data subject has requested an erasure.

(4) In case such personal data was made public, data controller shall take all reasonable steps, keeping in mind the available technology, to ensure any copies, links or duplication of the personal data is erased.

(5) Where personal data is requisite for purposes of:

(i) civil or criminal justice enforcement;

(ii) compliance with a legal obligation by a data controller;

(iii) public interest in relation to public health, statistics, scientific or historical research purposes and the erasure is likely to substantially diminish the purpose of processing; or

(iv) promoting the right to information and freedom of expression exercised in accordance with section 3 (2) (iii) of this Act.

The data controller may refrain from erasing those personal data, instead, restrict the processing to allow the achievement of the above mention in sub section (5) purposes respectively.

(6) Notwithstanding the provision of subsection (2)(3)(4) and (5) above, where the data controller is unable or refuses to comply with the request of the data subject, the data controller shall inform the data subject within 30 days of the receipt of the request, in writing, the reasons for such inability or refusal;

(7) The data subject, if aggrieved by the decision of the data controller or data processor under subsection (4) may institute a complaint to the Commission for redress in accordance with the provisions of this Act.

**Commercial Use of Personal Data**

39.(1.) Pursuant to section 38 it shall be unlawful for any person to use personal data for commercial purposes unless the person has sought and obtained written consent from the data subject;

(2) After complying with the provisions of subsection (1), the person who uses such data shall adopt all measures possible to remove identifiers or anonymise the personal data to the extent that the data subject is no longer identifiable.